**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Saba – Tarehe 16 Septemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

Taarifa ya Serikali kuhusu Taarifa ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2019 - 2020.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Taarifa ya Serikali kuhusu Taarifa ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2019 -2020.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe:**

Taarifa ya Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe kuhusu Malalamiko kutoka kwa Dkt. Hassan Rashid Ali dhidi ya Mhe. Ali Suleiman Ameir.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

140. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kufuatia ajali ya MV Spice ya mwaka 2011, Serikali ilipokea michango na rambi rambi kwa ajili ya kuwafariji waathirika. Hata hivyo, hadi leo bado waathirika au familia za waathirika hawajapatiwa fidia zao kutoka bima wala rambi rambi zilizokusanywa.

(a) Je, ni kiasi gani cha rambi rambi na malipo ya bima yalikusanywa kwa ajili ya kuwalipa fidia waathirika wa ajali hiyo.

(b) Je, ni lini na kwa viwango gani waathirika wa ajali hiyo watalipwa fidia zao kama ilivyotangazwa.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

113. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni jambo jema kwamba Serikali ilifanya ukarabati mkubwa na kuboresha jumba la biashara la Darajani ambalo milango yake imekodishwa wafanyabiashara mbali mbali kuendesha shughuli zao. Hata hivyo, inasikitisha kuona kwamba kuna Mamlaka za Serikali au kwa niaba ya Serikali zimeanzisha biashara ya kuzikodisha sehemu za maegesho, hali ambayo inasababisha usumbufu wa kukosekana kwa maegesho kwa wafanyabiashara na wateja wao.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kutoyaingilia maegesho ya magari yaliyopo mbele ya Jumba la Treni la Darajani ili kuongeza ufanisi wa ufanyaji biashara hapo.

(b) Je, ni kwa sheria ipi Serikali imenyang’anya maegesho hayo kutoka kwa wafanyabiashara waliopangishwa katika jengo hilo.

(c) Ni kigezo gani kimetumika kuweka bei ya kuegesha gari ndani ya Zanzibar ukilinganisha na kipato cha wastani cha Mzanzibari.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

81. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa katika kazi za Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu za Serikali duniani kote, wataalamu wenye taaluma za Certified Public Accountant – CPA hutambulika kutokana na umuhimu wao.

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua umuhimu wa taaluma hii.

(b) Je, ni wataalamu wangapi wanaotambulika na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wenye taaluma hiyo.

(c) Je, ni taasisi ngapi za Serikali zenye wataalamu hawa.

82. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha mifumo mbali mbali ya ukusanyaji wa mapato yake kupitia taasisi mbali mbali.

(a) Je, hadi hivi sasa Serikali ina mifumo mingapi ya ukusanyaji wa mapato.

(b) Je, mifumo hiyo ina uhusiano gani na mfumo mkuu wa ukusanyaji wa mapato Serikalini.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

8. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Baadhi ya wananchi wa shehia za Kama, Chuini na Kihinani katika jimbo la Mfenesini, wanaojishughulisha na kazi ya uvuvi, hukumbwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya uvuvi kama boti, nyavu na vifaa vyenginevyo.

(a) Kwa kuwa moja ya lengo kuu la Serikali ni kuwapatia wananchi maisha bora na kuwapunguzia umaskini Je,

Serikali ipo tayari kuwapatia vifaa hivyo wananchi wa shehia hizo ili waweze kujitegemea.

(b) Katika maeneo ya shehia za Kama na Kihinani, wapo pia wananchi wanaofanya biashara ya uvuvi na uuzaji wa dagaa. Je, Serikali imejiandaa vipi kuwasaidia wananchi hao.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

6. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika marekebisho ya katiba ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Shirikisho hilo limerejesha ngazi ya uongozi kwa Mkoa iliyoondolewa takriban miaka 30 iliyopita baada ya kuonekana kwamba ngazi hiyo haina kazi za kufanya isipokuwa kuendeleza urasimu tu.

(a) Kwa kuwa Katiba ya ZFF haiwezi kufanya kazi hadi ipitiwe na kuridhiwa na Msajili wa Vyama vya Michezo, Je, ni sababu zipi zilizopelekea Serikali kukubali kurejeshwa kwa ngazi hiyo ya Mkoa.

(b) Kwa kuwa vilabu vyote vimesajiliwa katika Wilaya zao, ni vyanzo gani vya fedha ambavyo vinategemewa na ofisi za ZFF za Mkoa.

37. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mashindano ya ngalawa yaliakisi utamaduni halisi wa Zanzibar na ule wa nchi za jahazi kwa ujumla, na nidhahiri kuwa mashindano hayo kwa sasa yameanza kupotea katika kila eneo Unguja na Pemba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza utamaduni wetu kwa kuyafufua na kuyaimarisha mashindano hayo.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

127. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kuna transfoma ya umeme iliyopo karibu na vijiji vya Mtakao, Mlindo ya Ngala na Kibendera katika jimbo la Pandani. Hata hivyo, hadi sasa vijiji hivi vimekosa kuungiwa huduma ya umeme kwa kukosekana nguzo zisizozidi sita kutoka eneo la umeme ulipo. Kwa kuwa Serikali kupitia viongozi wakuu imewaahidi wananchi hawa mara kadhaa juu ya kuwasogezea umeme.

(a) Je, ni kitu gani kimesababisha kutopelekewa umeme wananchi hawa.

(b) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi za viongozi wakuu wa nchi ya kuwasogezea wananchi wa Mtakao, Mlindo ya Ngala na Kibendera.

(c) Kwa vile makisio ya umeme kutoka skuli ya Dodeani kwenda Kichangani na Mlindo ya Ngala yalishafanyika tokea Januari, 2021 kufuatia ahadi ya Dkt. Shein, Rais mstaafu, Je, umeme utakuwa umefika wapi ifikapo Januari, 2022.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

23. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika miaka ya nyuma kisiwa cha Pemba kilikuwa kikiongoza kwa uzalishaji wa mihogo yenye sifa kubwa ya utamu pamoja na viazi vitamu vyenye sifa na kiwango bora. Lakini kwa miaka ya karibuni, viazi vimekuwa vikiagizwa kutoka Tanga kutokana na uzalishaji wa mazao haya kisiwani Pemba kupungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kushambuliwa na ugonjwa unaofanya majani ya muhogo kuwa na jasi jingi (cassava mealybug) kunakopelekea uzalishaji kuwa mdogo na muhogo kuwa mchungu.

Je, ni lini Serikali itaelekeza nguvu zake kuwasaidia wakulima wa Pemba kupambana na mdudu huyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

84. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya Vitongoji - Kibokoni ni ya muda mrefu, ni mbovu na chakavu sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo.

149. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais wa awamu ya nane aliyoitoa wakati wa ziara yake katika jimbo la Mtambile ya ujenzi wa barabara ya Mtambile hadi Jaani, Mjimbini hadi Mtondooni na Kangani hadi Kukuu kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini barabara hizo zitajengwa ili ziwasaidie wananchi na madereva wanaozitumia.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

148. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kutokana na ukiukwaji wa baadhi ya taratibu na sheria kwa baadhi ya wawekezaji wa mahoteli kuwazuia wananchi kufanya shughuli zao ikiwemo mazoezi, kuogolea na kutembea n.k.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara husika inalitambuwa hilo.

(b) Kama inalitambua suala hilo Je, Serikali imechukuwa hatua gani.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

99. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Asilimia thamanini (80) ya wakaazi wa kisiwa cha Pemba wamewekeza maisha yao katika sekta ya uvuvi. Kwa kuwa wavuvi wetu bado wanaendelea kutumia uvuvi ule ule wa zamani jambo ambalo linapelekea kuwakosesha mapato kwa lengo la kujipunguzia umasikini.

Je, ni lini Serikali yetu ya Zanzibar itakiagiza Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kuanzisha kitengo cha Sayansi ya Bahari na Uvuvi Tawi la Pemba (Faculty of Marine Science and Fishing Pemba Branch)

109. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali kwa mikakati yake ya kuongeza ufanisi na ufaulu kwa wanafunzi. Licha ya mikakati hiyo bado skuli za msingi za jimbo la Micheweni zimekuwa na changamoto ya kuvuja mapaa, uchache wa walimu wa kufundisha, skuli hizo kama vile skuli ya msingi na Maziwang'ombe na Shumba mjini n.k.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuondosha changamoto hizo ambazo zinarejesha nyuma maendeleo ya ufaulu kwa skuli za jimbo la Micheweni.

(b) Je, Wizara imeshawahi kuzitembelea skuli hizo na kuona ukubwa wa tatizo lenyewe.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

132. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha afya za wananchi kwa kuwapatia huduma mbali mbali zikiwemo huduma za matibabu ya moyo. Hata hivyo, kumekuwa na wazee katika jimbo la Pandani waliokata tamaa kwa kukosa matibabu ya watoto wao wenye matatizo ya moyo.

(a) Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuwashughulikia watoto wenye matatizo ya moyo ambao wazee wao hawana uwezo wa kuwatibu.

(b) Je, kwa sasa Zanzibar ina watoto wangapi walioripotiwa kuwa na matatizo ya moyo ambayo yameshindikana kutibiwa ndani ya Zanzibar.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

25. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika kipindi cha msimu huu wa karafuu, Serikali imeamua kufanya marekebisho ya bei ya zao hilo katika daraja zote tatu. Kubadilisha mfumo wa ununuzi wa zao hilo baada ya kulipa

fedha taslim, malipo hayo sasa yatalipwa kwa mkulima kupitia benki au mitandao ya simu. Kwa kuwa utaratibu huu ni mpya na haujawahi kutokea tangu zao hili lilipoingizwa hapa Zanzibar mwaka 1785 na mfanyabiashara wa kioman Saleh Buhamirel.

(a) Je, utaratibu huu hautakuwa sababu ya wakulima kupoteza au kuibiwa fedha zao.

(b) Ni lini Serikali itateremka katika ngazi za shehia kwa ajili ya kutoa mafunzo juu ya mauzo na manunuzi ya karafuu kupitia hesabu za benki (Benki Accounts) pamoja na mitandao ya simu.

## III. TAARIFA ZA SERIKALI

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

Taarifa ya Serikali kuhusu Taarifa ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2019 - 2020.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe:**

Taarifa ya Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe Kuhusu Malalamiko kutoka kwa Dkt. Hassan Rashid Ali dhidi ya Mhe. Ali Suleiman Ameir.

**Zanzibar,**
**16 Septemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**